HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

MUHTASARI WA MKUTANO WA KWANZA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA TAREHE 14/12/2020 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA STENDI YA MSAMVU

Wajumbe waliohudhuria

1.	Mhe. Pascal M. Kihanga	__	Mstahiki Meya – Mwenyekiti
2.	Ndg.Ndg. Sheilla E. Lukuba	__	Mkurugenzi wa Manispaa – Katibu
3.	Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele	__	Naibu Meya – Mjumbe
4.	Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood(Mb)	__	Mjumbe
5.	Mhe. Dr. Christine Ishengoma(Mb)	__	Mjumbe
6.	Mhe. Norah Mzeru(Mb)	__	Mjumbe
7.	Mhe. Ally Rashid Kalungwana	__	Mjumbe
8.	Mhe. Madaraka S. Bidyanguze	__	Mjumbe
9.	Mhe. Rashid Ramadhani Matessa	__	Mjumbe
10.	Mhe. Dr. Joel Albart Kisome	__	Mjumbe
11.	Mhe. Amina H. Zihuye	__	Mjumbe
12.	Mhe. Hadija Kombo Kibati	__	Mjumbe
13.	Mhe. Zamoyoni J. Abdallah	__	Mjumbe
14.	Mhe. Rahma Lashayo Maumba	__	Mjumbe
15.	Mhe. Eng. Hamisi Ndwata	__	Mjumbe
16.	Mhe. Amini Abdallah Tunda	__	Mjumbe
17.	Mhe. Selestini Savin Mbilinyi	__	Mjumbe
18.	Mhe. Hamisi Ally Kilongo	__	Mjumbe
19.	Mhe. Abdallah Ally Meya	__	Mjumbe
20.	Mhe. Thomas Benedict Butabile	__	Mjumbe
21.	Mhe. Samueli Alfred Msuya	__	Mjumbe
22.	Mhe. Namala Johaness Mchunguzi	__	Mjumbe
23.	Mhe. Athuman Omary Lujuo	__	Mjumbe
24.	Mhe. Salum Mrisho Chunga	__	Mjumbe
25.	Mhe. Majuto Athumani Mbuguyu	__	Mjumbe
26.	Mhe. Marco Mathias Kanga	__	Mjumbe
27.	Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu	__	Mjumbe
28.	Mhe. Zuber George Mkalaboko	__	Mjumbe

29.	Mhe. Mwanaidi A. Ngulungu	__	Mjumbe
30.	Mhe. Juma Issa Kiduka	__	Mjumbe
31.	Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani	__	Mjumbe
32.	Mhe. Merichior Peter Mwamnyanyi	__	Mjumbe
33.	Mhe. Emmy Kiula Rajabu	__	Mjumbe
34.	Mhe. Peter Joel Dhahabu	__	Mjumbe
35.	Mhe. Hassan Madadi Maringo	__	Mjumbe
36.	Mhe. Lt.Col. (MST) Ahmed Salum Mazora	__	Mjumbe
37.	Mhe. Salma Bonzo Mbandu	__	Mjumbe
38.	Mhe. Zinduna Kombo Sulemani	__	Mjumbe
39.	Mhe. Seif Zahoro Chomoka	__	Mjumbe
40.	Mhe. Aisha Ahmad Kitime	__	Mjumbe
41.	Mhe. Grace L. Mkumbae	__	Mjumbe
42.	Mhe. Warda O. Bazia	__	Mjumbe
43.	Mhe. Latifa Saidi Ganzel	__	Mjumbe

Watendaji waliohudhuria

1.	Ndg. Pilly Kitwana	__	Afisa Utumishi wa Manispaa
2.	Dr. Tito Kagize	__	Afisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa
3.	Ndg. Michael Waluse	__	Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Manispaa
4.	Ndg. Jeremiah Lubeleje	__	Mchumi wa Manispaa
5.	Ndg. Adam T. Shayo	__	Mthibiti Ubora wa Shule Wilaya
6.	Ndg. Asteria L. Mwang'ombe	__	Afisa Michezo
7.	Ndg. Jafari A. Makupula	__	Afisa Manunuzi na Ugavi wa Manispaa
8.	Ndg. Neema Michael	__	Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa
9.	Ndg. Samuel Subi	__	Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu wa Manispaa
10.	Ndg. Chausiku Masegenya	__	Afisa Elimu Msingi wa Manispaa
11.	Dkt. Janeth Barongo	__	Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa
12.	Ndg. Feliciana Katemana	__	Mratibu wa TASAF wa Manispaa
13.	Ndg. Kitutu Mshana	__	Afisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Manispaa
14.	Eng. Juma Gwisu	__	Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Manispaa
15.	Ndg. Ponceano P. Kilumbi	__	Mweka Hazina wa Manispaa
16.	Ndg. Nesphora Kinoge	__	Kaimu Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa
17.	Ndg. Majubu F. Mkama	__	Kaimu Katibu TSC wa Manispaa
18.	Ndg. Enedy Mwanakatwe	__	Afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa

19.	Ndg. Emeline E. Kihunrwa	__	Kaimu Afisa Mipangomiji na Maliasili wa Manispaa
20.	Ndg. Hamisi Ally	__	Kaimu Afisa Tarafa wa Manispaa
21.	Ndg. Safia Kingwahi	__	Afisa Utamaduni wa Manispaa
22.	Ndg. Festus Herman	__	Afisa Biashara wa Manispaa
23.	Dr. Ikaji Z. Rashid	__	Mganga Muu wa Afya wa Manispaa
24.	Ndg. Shaban R. Duru	__	Afisa Usafirishaji wa Manispaa
25.	Ndg. Suzan Kimambo	__	Afisa Usafirishaji
26.	Ndg. Jacqueline Mushi	__	Afisa Maendeleo ya Jamii
27.	Ndg. Elikarim S. Tyeah	__	Kaimu Mwanasheria wa Manispaa
28.	Ndg. Pendo S. Chagu	__	Afisa Uchaguzi wa Manispaa

Waalikwa waliohudhuria

1.	Eng. Emmanuel N.M. Kalobelo	__	Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro
2.	Mhe. Bakari Msulwa	__	Mkuu wa Wilaya ya Morogoro
3.	Mhe. Fikiri H. Juma	__	Mwenyekiti wa CCM Wilaya
4.	Ndg. Ruth John	__	Katibu Tawala Wilaya ya Morogoro
5.	Ndg. Zainab Kissoky	__	Afisa Maadili
6.	Mhe. S.J. Nganga	__	Hakimu Mahakama ya Mwanzo Nunge
7.	Sheikh Ramadhani Rashid	__	BAKWATA Wilaya
8.	Ndg. Erasto Gowele	__	Afisa Usalama Wilaya
9.	Ndg. Sofia A. Kibaba	__	Katibu wa CCM Wilaya
10.	Ndg. Maulidi Chambilila	__	Katibu Mwenezi na Siasa CCM Wilaya
11.	Ndg. Leopold Ngirwa	__	Afisa wa Serikali za Mitaa Mkoa
12.	Ndg. Erasmus Haule	__	Afisa Usalama
13.	Ndg. Andrew Chimesela	__	Afisa Habari kutoka Ofisi ya RAS.

Sekretarieti

1.	Ndg. Daudi Kibwana	__	Katibu wa Mikutano
2.	Ndg. Deogratias Butabile	__	Katibu wa Mikutano
3.	Ndg. Theresia Mbena	__	Katibu wa Mikutano
4.	Ndg. Lilian Henerico	__	Afisa Habari
5.	Ndg. Sylvia Kahitwa	__	Katibu wa Mikutano

HMM/BM/1/ 2020/2021 Kufungua Kikao.

Kabla ya Mkutano kufunguliwa Viongozi wa Dini ya Kiislam na Kikristo waliomba Dua kuuombea Mkutano huo.

Dua hiyo iliombwa na Sheikh Ramadhan Rashid na Mhe. Mch. Thomas B. Butabile ambapo kwa pamoja walisisitiza Amani, Utulivu na Ushirikiano miongoni mwa Madiwani kwa Madiwani, Madiwani na Watendaji katika kuiletea maendeleo Halmashauri.

Ufunguzi wa Mkutano

Mkurugenzi wa Manispaa alieleza kuwa kwa mujibu wa Kanuni 7(2) ya Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro za mwaka 2016 inaeleza kuwa "Mkutano wa kwanza wa uchaguzi wa Meya, Naibu Meya na Wajumbe wa Kamati utaongozwa na Katibu Tawala wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa Katibu. Kutokana na Kanuni hiyo, Mkurugenzi wa Manispaa alimkaribisha Ndugu Ruth John Katibu Tawala Wilaya ili afungue Mkutano.

Mwenyekiti wa muda aliwakaribisha Wajumbe na aliwapongeza kwa ushindi walioupata wa asilimia 100 na kuwaomba watimize ahadi zao walizozitoa kwa Wananchi.

Alifungua Mkutano saa 4:30 asubuhi.

Nasaha za Mkuu wa Wilaya

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro aliwapongeza Waheshimiwa Madiwani kwa uchaguzi na ushindi wa asilimia 100, na pia Manispaa kuongoza kimkoa katika kura za Rais kwa asilimia 99.6. Aliomba Mstahiki Meya atakayechaguliwa apewe ushirikiano kwa maendeleo ya Halmashauri.

Aliagiza Baraza la Madiwani lihakikishe linasimamia na kutekeleza agizo la Serikali linaloelekeza kwamba ifikapo mwishoni mwa mwezi Februari, 2021 vyumba vya madarasa ya Sekondari ambapo kwa Manispaa ya Morogoro kuna upungufu wa vyumba 25 vinakamilika ujenzi ili kuwezesha Wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Sekondari wanaanza shule.

HMM/BM/2/ 2020/2021 Kuridhia agenda za Mkutano.	Wajumbe waliridhia agenda zifuatazo:- 1) Kufungua Mkutano 2) Madiwani wateule kula kiapo. 3) Waheshimiwa Madiwani kusaini fomu za ahadi ya uadilifu kwa Watumishi wa Umma mbele ya Kamishna wa Maadili. 4) Kumchagua Mstahiki Meya na Naibu Meya wa Halmashauri 5) Kuunda Kamati za Kudumu za Halmashauri kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022. 6) Madiwani kuwasilisha anuani za makazi yao ya kudumu ikiwemo namba za simu kwa Mkurugenzi wa Manispaa kwa ajili ya kupokea taarifa 7) Kupitisha ratiba ya mikutano na vikao kwa mwaka wa fedha 2020/2021. 8) Kupokea taarifa ya Mkurugenzi wa Manispaa kuhusu kumbukumbu ya maamuzi ya utekelezaji wa shughuli za Halmashauri zilizofanyika katika kipindi ambacho Baraza la Madiwani lilivunjwa 9) Kufunga Mkutano
HMM/BM/3/ 2020/2021 Madiwani Wateule kula kiapo.	Mheshimiwa S.J. Nganga - Hakimu Mkazi wa Mahakama ya mwanzo Nunge aliwaapisha Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ambapo watahudumu kwa kipindi cha miaka mitano (2020-2025).
HMM/BM/4/ 2020/2021 Waheshimiwa Madiwani kusaini fomu za ahadi ya uadilifu kwa Watumishi wa Umma mbele ya Kamishna wa Maadili.	Waheshimiwa Madiwani walisaini fomu za ahadi ya uadilifu kwa Watumishi wa Umma mbele ya Kamishna wa Maadili.

HMM/BM/5/ 2020/2021 Kumchagua Mstahiki Meya na Naibu Meya wa Halmashauri

Ilielezwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 7(2) ya Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro za mwaka 2016, Katibu Tawala Wilaya(Mwenyekiti) alitoa mwongozo wa Uchaguzi wa Mstahiki Meya na Naibu Meya wa Halmashauri ambapo alieleza kuwa uchaguzi utakuwa ni wa siri hivyo kila Mjumbe atapiga kura za siri. Aidha, kila Mjumbe ataitwa na kujaza fomu maalum.

Uchaguzi wa nafasi ya Mstahiki Meya na Naibu Meya:-

Mkurugenzi wa Manispaa alisoma barua yenye kumbukumbu Na. CCM/DHQ/UR/M/Vol.1/158/53 ya tarehe 04/12/2020 kutoka kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya akiwatambulisha Mhe. Pascal M. Kihanga kuwa Mgombea wa nafasi ya Mstahiki Meya wa Halmashauri kwa kipindi cha mwaka 2020/2025 na Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele kuwa Naibu Meya wa Halmashauri kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 (kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni ya 7(4) ya Kanuni za kudumu za Halmashauri za mwaka 2016).

Kwa kuwa Baraza la Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro linaundwa na Madiwani wa Chama kimoja cha Mapinduzi (CCM), Wajumbe watapiga kura za Ndiyo au Hapana.

Kabla ya Uchaguzi, Mwenyekiti aliwapa muda wa dakika 3 kila mgombea ili kuomba kura kwa Wajumbe.

Baada ya Wagombea kuomba kura, kura za siri zilipigwa na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

1. Uchaguzi wa nafasi ya Naibu Meya kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 kwa mujibu wa Kanuni ya 7(4) ya Kanuni za Kudumu za Halmashauri za mwaka 2016

i) Jina la mgombea – Mhe. Mohamed Y. Lukwele

- Wajumbe waliopiga kura 42
- Kura zilizoharibika 0
- Kura halali za Ndiyo 42 sawa na asilimia 100

Kwa mamlaka aliyopewa, Ndugu Ruth John Katibu - Tawala Wilaya (Mwenyekiti) alimtangaza Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele kuwa Naibu Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022.

2. Uchaguzi wa nafasi ya Mstahiki Meya kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025:-

ii) Jina la mgombea Mhe. Pascal M. Kihanga

- Wajumbe waliopiga kura 42
- Kura zilizoharibika 0
- Kura halali za ndiyo 42 sawa na asilimia 100

Kwa mamlaka aliyopewa, Ndugu Ruth John – Katibu Tawala Wilaya (Mwenyekiti) alimtangaza Mhe. Pascal M. Kihanga kuwa Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa kipindi cha miaka mitano. (2020-2025)

Wajumbe wote waliwapongeza Viongozi waliochaguliwa na kuahidiwa kupewa ushirikiano ili kuiletea maendeleo Halmashauri

HMM/BM/6/ 2020/2021 Kuunda Kamati za Kudumu za Halmashauri kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022

Mstahiki Meya kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Manispaa aliunda Kamati za Kudumu na Kamati nyinginezo kama ifuatavyo:-

1. KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI.

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya – Mwenyekiti
2)	Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele	Naibu Meya - Mjumbe
3)	Mhe. Abdulaziz Mohamed (MB)	Mjumbe
4)	Mhe. Eng. Hamis H. Ndwata	Mjumbe
5)	Mhe. Tunda A. Abdallah	Mjumbe
6)	Mhe. Zamoyoni J. Abdallah	Mjumbe
7)	Mhe. Salma Bonzo Mbandu	Mjumbe
8)	Mhe. Mwanaidi E. Ngulungu	Mjumbe
9)	Mhe. Peter Joel Dhahabu	Mjumbe
10)	Mhe. Marco Mathias Kanga	Mjumbe
11)	Mhe. Ally Rashid Kalungwana	Mjumbe

2. KAMATI YA HUDUMA ZA UCHUMI, ELIMU NA AFYA:

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1	Mhe. Amini Abdallah Tunda	Mwenyekiti
2	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya – Mjumbe
3	Mhe. Dr. Christine Ishengoma(Mb)	Mjumbe
4	Mhe. Abdallah Ally Meya	Mjumbe
5	Mhe. Thomas Benedict Butabile	Mjumbe
6	Mhe. Merichior Peter Mwamnyanyi	Mjumbe
7	Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu	Mjumbe

8	Mhe. Selestini Savin Mbilinyi	Mjumbe
9	Mhe. Emmy Kiula Rajabu	Mjumbe
10	Mhe. Namala Johaness Mchunguzi	Mjumbe
11	Mhe. Peter Joel Dhahabu	Mjumbe
12	Mhe. Seif Zahoro Chomoka	Mjumbe
13	Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani	Mjumbe
14	Mhe. Marco Mathias Kanga	Mjumbe
15	Mhe. Zamoyoni J. Abdallah	Mjumbe
16	Mhe. Amina H. Zihuye	Mjumbe
17	Mhe. Latifa Saidi Ganzel	Mjumbe
18	Mhe. Warda O. Bazia	Mjumbe
19	Mhe. Aisha Ahmad Kitime	Mjumbe
20	Mhe. Lt. Col. (Mst) Ahmed Salum Mazora	Mjumbe
21	Mhe. Rashid Ramadhani Matessa	Mjumbe

3. KAMATI YA MIPANGOMIJI NA MAZINGIRA:

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Eng. Hamis Hamad Ndwata	Mwenyekiti
2	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya – Mjumbe
3	Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood(Mb)	Mjumbe
4	Mhe. Norah Mzeru (Mb)	Mjumbe
5	Mhe. Hamisi Ally Kilongo	Mjumbe
6	Mhe. Samueli Alfred Msuya	Mjumbe
7	Mhe. Hassan Madadi Maringo	Mjumbe
8	Mhe. Zinduna Kombo Sulemani	Mjumbe
9	Mhe. Ally Rashid Kalungwana	Mjumbe
10	Mhe. Madaraka Steven Bidyanguze	Mjumbe
11	Mhe. Zuber George Mkalaboko	Mjumbe
12	Mhe. Juma Issa Kiduka	Mjumbe
13	Mhe. Athuman Omary Lujuo	Mjumbe
14	Mhe. Salum Mrisho Chunga	Mjumbe
15	Mhe. Dr. Joel Albart Kisome	Mjumbe
16	Mhe. Majuto Athumani Mbuguyu	Mjumbe
17	Mhe. Hadija K. Kibati	Mjumbe
18	Mhe. Salma Bonzo Mbandu	Mjumbe
19	Mhe. Grace L. Mkumbae	Mjumbe
20	Mhe. Mwanaidi E. Ngulungu	Mjumbe
21	Mhe. Rahma Lashayo Maumba	Mjumbe

4. KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI:

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Mohamed Yahaya Lukwele	Naibu Meya - Mwenyekiti
2)	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya - Mjumbe
3)	Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb)	Mjumbe
4)	Mhe. Norah Mzeru (Mb)	Mjumbe
5)	Mhe. Dr. Christine Ishengoma (Mb)	Mjumbe
6)	Mhe. Selestin S. Mbilinyi	Mjumbe
7)	Mhe. Abdallah Mohamed Chamgulu	Mjumbe
8)	Mhe. Latifa Saidi Ganzel	Mjumbe
9)	Mhe. Amina H. Zihuye	Mjumbe

5. KAMATI YA MAADILI:

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Emmy Kiula Rajabu	Mwenyekiti
2)	Mhe. Merichior Peter Mwamnyanyi	Mjumbe
3)	Mhe. Thomas Benedict Butabile	Mjumbe
4)	Mhe. Madaraka Steven Bidyanguze	Mjumbe
5)	Mhe. Zinduna Kombo Sulemani	Mjumbe

6. KAMATI NDOGO YA MAZINGIRA

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Dr. Joel Albart Kisome	Mjumbe
2)	Mhe. Eng. Hamis Hamadi Ndwata	Mjumbe
3)	Mhe. Hamisi Ally Kilongo	Mjumbe
4)	Mhe. Hassan Madadi Maringo	Mjumbe
5)	Mhe. Grace L. Mkumbae	Mjumbe
6)	Mhe. Athuman Omary Lujuo	Mjumbe

7. KAMATI YA KUGAWA ARDHI:

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Juma Issa Kiduka	Mjumbe
2)	Mhe. Warda O. Bazia	Mjumbe

8. MJUMBE WA MKUTANO MKUU WA AGM MSAMVU PROPERTIES:

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya
2)	Mhe. Seif Zahoro Chomoka	Mjumbe

9. MFUKO WA JIMBO:

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Abdul Aziz Mohamed	Mwenyekiti
2)	Mhe. Rahma Lashayo Maumba	Mjumbe
3)	Mhe. Salum Mrisho Chunga	Mjumbe
4)	Ndg. Bright D. Sospeter	WEO - Mjumbe
5)	Ndg. Martha Norasco Kipanga	WEO - Mjumbe

10. ALAT MKOA

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Pascal M. Kihanga	Mstahiki Meya
2)	Mhe. Abdulaziz Mohamed (Mb)	Mjumbe
3)	Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani	Mjumbe
4)	Mhe. Hadija K. Kibati	Mjumbe

11. BODI YA AJIRA

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Rashid R. Matessa	Mjumbe

12. BODI YA MORUWASA

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Lt. Col. (Mst) Ahmed Salum Mazora	Mjumbe

13. BODI YA NGOZI

NA	JINA KAMILI	NAFASI
1)	Mhe. Samueli Msuya	**Mjumbe**

Baraza lilimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa kufuatilia mamlaka husika kujua Bodi ya Ngozi inavyofanya kazi kwa kuwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita (2015-2020) Bodi hiyo haikufanya vikao.

HMM/BM/7/ 2020/2021 Madiwani kuwasilisha anuani za makazi yao ya kudumu ikiwemo namba za simu kwa Mkurugenzi wa Manispaa kwa ajili ya kupokea taarifa.	Waheshimiwa Madiwani waliwasilisha anuani za makazi yao ya kudumu na namba za simu katika daftari lililoandaliwa na Mkurugenzi wa Manispaa.
HMM/BM/8/ 2020/2021 Kupitisha ratiba ya mikutano na vikao kwa mwaka wa fedha 2020/2021	Ratiba ya Vikao na Mikutano ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa. Wajumbe walisisitiza kuwa makabrasha ya vikao yawe yanawafikia mapema Wajumbe kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Halmashauri za mwaka 2016.
HMM/BM/9/ 2020/2021 Kupokea taarifa ya Mkurugenzi wa Manispaa kuhusu kumbukumbu ya maamuzi ya utekelezaji wa shughuli za Halmashauri zilizofanyika katika kipindi ambacho	Taarifa ya maamuzi ya shughuli za Halmashauri zilizofanyika katika kipindi ambacho Baraza la Madiwani lilivunjwa iliwasilishwa na ilipokelewa kisha Wajumbe waliiridhia.

Baraza la Madiwani lilivunjwa

HMM/BM/10/ 2020/2021 Kufunga kikao.

Kabla Mkutano haujafungwa Mkuu wa Wilaya alimkaribisha Katibu Tawala Mkoa ili atoe salamu za Mkuu wa Mkoa wa Morogoro kisha azindue Baraza la Madiwani.

Katibu Tawala Mkoa alisoma Hotuba na alishauri Baraza la Madiwani kutekeleza yafuatayo:-

i) Kudumisha Ulinzi, Amani na Utawala Bora.

ii) Kuimarisha huduma za kijamii na Uchumi wa Wananchi.

iii) Kuimarisha maendeleo ya Wananchi kwa kuzingatia Sera na Mipango ya Nchi.

iv) Kuhakikisha kuwa Waheshimiwa Madiwani wanasimamia kwa karibu ukusanyaji wa Mapato ya ndani kwa kuhamasisha ulipaji wa ushuru, ada na tozo mbalimbali kwa mujibu wa Sheria Ndogo za Halmashauri na Sheria zingine zilizopo. Aidha ilisisitizwa kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa kutumia fursa zilizopo katika Halmashauri ikiwa ni pamoja na kufanya uwekezaji katika miradi ya kimkakati ya uwekezaji ili Halmashauri iweze kujitegemea.

v) Kusimamia na kuhakikisha fedha zinazokusanywa na Halmashauri na katika vituo vya kutolea huduma zinawekwa Benki kabla ya kutumika.

vi) **Kuhusu utengaji wa fedha za maendeleo kutoka kwenye mapato ya ndani.**

Kuhakikisha fedha za mapato ya Ndani asilimia **60** ambapo asilimia **50** miradi ya maendeleo na asiimia 10 za vikundi vya Wanawake, vijana na Watu wenye Ulemavu zinapelekwa kwenye Akaunti maalum kadri zinavyokusanywa kama ilivyoelekeza Serikali.

vii) Kuhusu lishe

Halmashuri isimamie utoaji wa **Tshs. 1,000.00** kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano (5) kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri kila mwaka kama ilivyoelekeza Serikali kwa ajili ya Lishe.

viii) Kuhusu Wananchi kuhamasishwa kujiunga na mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Wananchi waendelee kuhamasishwa kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (CHF) ili Wananchi waweze kupata huduma ya

Afya kikamilifu. Aidha Serikali itaendelea kutenga dawa za kutosha kuhudumia Wananchi watakaojiunga na mfuko huo.

ix) **Kuhusu uwepo wa matukio mengi ya kikatili kwa watoto yakihusisha kingono na kiuchumi:-**

Halmashauri ibuni mikakati ili kuondoa ukatili huo ili kujenga jamii yenye ustawi na maendeleo binafsi na Taifa kwa ujumla.

x) Kuhusu matokeo ya mtihani wa darasa la saba mwaka 2020.

Alitoa pongezi kwa viongozi, walimu, wanafunzi, wazazi na walezi pamoja na wadau mbalimbali wa elimu katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kutokana na jitihada walizofanya katika sekta ya elimu na kuuwezesha Mkoa kuinua ufaulu katika Mtihani wa kumaliza darasa la saba mwaka 2020 ambapo Wanafunzi **52,640** walifanya Mtihani huo na wanafunzi **45,457** walifaulu. Hivyo Mkoa wa Morogoro umepata ufaulu wa asilimia **87.21** kutoka asilimia **78.49** mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la asilimia **8.72**.

Hali hiyo imeuwezesha Mkoa kuingia kwenye mikoa kumi bora kitaifa mwaka 2020 kwa kushika nafasi ya **8** kutoka nafasi ya **16** mwaka 2019.

Baada ya Mkoa wa Morogoro kuingia kwenye kumi bora aliiagiza Halmashauri kuongeza kasi katika Elimu kwani matokeo ya Mtihani wa kumaliza Darasa la saba mwaka 2020 mbali ya kuongeza kiwango cha ufaulu wa asilimia **1.66** kwa kuwa na ufaulu wa asilimia **90.57** mwaka 2020 kutoka asilimia **88.91** mwaka 2019, hivyo Halmashauri imekuwa ya **4** Kimkoa mwaka 2020 wakati mwaka 2019 ilishika nafasi ya tatu Kimkoa.

Kutokana na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wa kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) – 2020, mahitaji ya vyumba vya madarasa kwa kidato cha kwanza (I) – 2021 yameongezeka kwa ngazi ya Mkoa pia kwa ngazi ya Halmashauri.

Kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro vinahitajika kujengwa vyumba vya madarasa ya kidato cha kwanza 25 ili vikamilike ifikapo tarehe 28/02/2021 na kuwezesha wanafunzi wote waliofaulu kuwa darasani.

Aidha, Serikali ilishatoa maelekezo kwa Wakuu wa Wilaya na Halmashauri kuhakikisha vyumba hivyo vya madarasa vinajengwa na kuwekwa madawati yote.

xi) Kuhusu uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia Sekta za Kilimo Mifugo, Ushirika, Viwanda na Biashara Halmashauri iliagizwa itekeleze yafuatayo:-

- Kuhimiza uanzishajina uendelezajiwa maeneo ya kimkakati ndani ya Manispaa.
- Kuhimiza uanzishaji wa vikundi mbalimbali vya uzalishaji wa mali kwa mfumo wa Kilimo Nyumba (GREEN HOUSE).
- Kuhimiza uanzishaji na uendelezaji wa Viwanda kwa ajili ya uchakataji na uongeaji wa thamani katika mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na ufugaji wa Nyuki.
- Kuhimiza na kuweka vivutio kwa wawekezaji katika sekta mblimbali za uzalishaji ikiwa ni pamoja a kujenga "ONE STOP CENTRE".
- Kuhimiza utoaji wa vitambulisho vya Wajasiriamali
- Kuhimiza uwepo wa Mazingira, wezeshi kwa wawekezaji na Wafanyabiashara.

xii) Kuhusu migogoro ya Ardhi:

- Kuhakikisha migogoro ya ardhi inadhibitiwa na kushugulikiwa kwa wakati
- Kusimamia utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi wa majengo yaliyopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kuhimiza na kusimamia upimaji wa viwanja na kuweka miundombinu muhimu katika viwanja vilivyopimwa kama vile barabara, maji na umeme.
- Kuhimiza usafi wa Mazingira ikiwemo kufanya usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.
- Halmashauri inaweza kutenga fedha katika mapato ya ndani kwa ajili ya barabara. Aidha Halmashauri ishirikiane na TARURA kuboresha barabara.
- Kuhakikisha miradi ya maendeleo inakamilika kwa wakati kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa.
- Kuhimiza masuala ya hifadhi mazingira na usimamizi wa Maliasili
- Kila Diwani apewe Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025

xiii) Kuhusu mikopo ya Waheshimiwa Madiwani:-
Serikali ilikwisha weka utaratibu kuwa Mikopo itolewe siyo zaidi ya theluthi mbili ($^2/_3$) ya posho ya Madiwani kwa mwezi na msisitizo, ulitolewa urejeshwaji wa mikopo katika Benki husika ifanyike kwa wakati.

Baada ya Hotuba hiyo Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro alitamka rasmi kuzindua Baraza la Madiwani la Manispaa ya Morogoro la mwaka 2020.

Baada ya Baraza kuzinduliwa Mstahiki Meya alimshukuru Katibu Tawala Mkoa kwa maagizo yake kwa Halmashauri na kuahidi kuyasimamia katika utekelezaji. Baada ya kusema hayo alifunga Mkutano saa 11:15 jioni.

Muhtasari umethibitishwa tarehe……

……	……
Mhe. Pascal M. Kihanga	Ndg. Sheilla E. Lukuba
MSTAHIKI MEYA	**MKURUGENZI WA MANISPAA**
MWENYEKITI	**KATIBU**

YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAWAIDA CHA MENEJIMENTI (CMT) KILICHOFANYIKA TAREHE 04/11/2020

MUHT NA.	MAELEZO	MTEKELE ZAJI	UTEKELEZAJI